Julai 17, 2026 Pg 13

# LATRA ionekane vizuri kona zote, kusimamia usafiri na kukagua ada



Na Christina Mwakangale

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepewa jukumu la kusimamia sekta ya usafiri nchini kwa kuhakikisha huduma zinakuwa salama, zenye ubora, zinazopatikana kwa urahisi na zinazozingatia haki za abiria.

Sheria ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo pia inaipa wajibu wa kuratibu usalama wa usafiri, kusimamia viwango vya huduma, kushughulikia malalamiko ya wananchi na kudhibiti nauli pamoja na masharti ya utoaji wa huduma.

Hivi karibuni kumekuwa na ukaguzi kwa vyombo vya usafiri mijini hasa bodaboda na bajaji, jambo linalofanya makundi hayo mawili kukwepana.

Abiria wanaotumia usafiri huo, wanashuhudia yote hayo pale maofisa hao wanapofika mbele ya bajaji au bodaboda kwenye makutano ya barabara au taa za kuongozea vyombo vya usafiri.

Hata hivyo, kwa mtazamo wa wananchi wengi, picha inayoonekana mitaani ni tofauti. Siku hizi ni jambo la kawaida kuwaona wasaidizi wa LATRA katika vituo vya bodaboda wakifanya ukaguzi wa kama madereva wamelipia ada na kutimiza masharti ya usajili.

Hatua hiyo ni muhimu katika kuhakikisha sekta inafanya kazi kwa kufuata sheria, lakini inazua swali moja la msingi; je, mamlaka hiyo imejikita kwa kiwango hicho hicho katika kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa kwa abiria?

> **Usafiri wa umma haupaswi kupimwa kwa idadi ya leseni zilizotolewa au ada zilizokusanywa pekee. Unapaswa kupimwa kwa ubora wa huduma anayopata mwananchi.**

Katika Jiji la Dar es Salaam, changamoto za usafiri wa umma bado ni nyingi. Abiria hukumbana na makondakta wanaotumia lugha za matusi, madereva wanaoendesha kwa mwendo wa hatari, magari yanayokata njia kabla ya kufika mwisho wa leseni zao, pamoja na tabia ya kupandisha nauli kinyume na viwango vilivyowekwa.

Haya ni mambo yanayowagharimu wananchi kila siku, lakini mara nyingi hatua za udhibiti hazionekani kwa kiwango kinachotarajiwa.

Mfano halisi ni katika Kituo cha Mwenge, Dar es Salaam, nyakati za jioni. Wakati maelfu ya wafanyakazi na wanafunzi wanapohitaji kurejea nyumbani, idadi ya daladala hupungua kwa kiasi kikubwa., daladala zingine zinapaki kituoni hapa mithiri ni kituo maalum kwa ajili ya maegesho, abiri wakiuliza wanajibu 'HATUENDI' GARI MBOVU'.

Baada ya muda daladala hiyohiyo unaikuta barabarani ikienda ruti fupi ambayo sio yake. Kama ni ya Mwnge - Gongolamboto, itabeba abiria iishie Buguruni, kisha apakie tena Buguruni-Gongolamboto.

Abiria hulazimika kusubiri kwa muda mrefu, huku baadhi ya magari yakikwepa njia zao za kawaida au kutoingia kabisa kituoni.

Matokeo yake ni msongamano mkubwa, usumbufu na wakati mwingine ulazima wa kulipa nauli kubwa kuliko iliyopangwa ili kuwahi kufika nyumbani.

Usafiri wa umma haupaswi kupimwa kwa idadi ya leseni zilizotolewa au ada zilizokusanywa pekee. Unapaswa kupimwa kwa ubora wa huduma anayopata mwananchi.

Abiria anahitaji usalama, heshima, usafi wa vyombo vya usafiri, uhakika wa kupata gari kwa wakati na huduma inayozingatia utu.

LATRA kuongeza nguvu katika ukaguzi wa ubora wa huduma. Maofisa wake wanapaswa kuwepo kwenye vituo vikubwa na ndani ya magari ili kufuatilia mwenendo wa madereva na makondakta, kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka masharti ya leseni na kuhakikisha ratiba za usafiri zinafuatwa.Malalamiko ya wananchi yashughulikiwe kwa haraka na hatua zilizochukuliwa ziwekwe wazi ili kuongeza uwajibikaji.

Ripoti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT), pia imebainisha changamoto za usafiri wa mijini, ikiwamo muda mrefu wa kusubiri usafiri, kupandishwa kwa nauli na udhaifu wa usimamizi, huku ikipendekeza kuimarishwa kwa udhibiti na uratibu wa sekta.

LATRA haliishii kukagua vibandiko vya ada kwenye bodaboda. Wananchi wanatarajia kuona mamlaka inayosimamia usafiri kwa ukamilifu, inayolinda haki za abiria na kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma salama, yenye hadhi na inayostahili katika kila safari.

CamScanner